


# HERI ILIYOSAHULIKA

 . . . tunakushukuru kutoka kwenye kilindi cha moyo wetu, kwa ajili ya Bwana Yesu, Yeye aliye Uzima wetu, na ndani Yake hatuoni makosa yoyote. Lakini tunaona ndani yetu, makosa, tunapoyaangalia maisha Yake na kuyachunguza, yetu kwa Yake, tunaomba ya kwamba utusamehe.

<sup>2</sup> Tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba Wewe utakutana nasi. Uliahidi ya kwamba popote wawili au zaidi watakapokutana pamoja, ya kwamba Wewe ungekuwa katikati, na kama tungeomba chochote, kwamba tungepewa.

<sup>3</sup> Na, Baba, nia ye—yetu na kusudi letu, usiku wa leo, na shauku yetu moyoni mwetu ni kumwona Kristo ametukuzwa. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba jitihada zetu usiku wa leo zitakuwa, zinapoendelea, kuwaleta watu kwenye imani iliyo hai katika Mungu aliye hai, kwamba, Mungu ambaye hajafa, bali yu hai milele.

<sup>4</sup> Tunaomba Baba, ya kwamba utazichochea nafsi zetu usiku wa leo, kwa Uwepo Wako, kupitia Yesu Kristo, tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

<sup>5</sup> Mnaweza kuketi. Nimechelewa kidogo tu na kidogo nimechoka, nimekuwa nikienda tangu Krismasi bila kikomo, kwa hiyo nimechoka sana. Nilifurahi, usiku wa leo, kumwona Ndugu Joseph Boze, ambaye nimekuwa nikitazamia kumwona kwa muda fulani, akirudi kutoka hudumani ng'ambo ya bahari.

<sup>6</sup> Pia nasikitika kusema, usiku wa leo, ya kwamba ndugu yetu wa thamani na rafiki, hapa, Ndugu Tommy Hicks, anatuacha usiku wa leo kwenda, ama, kesho asubuhi kwenda Canada kuwa na mkutano. Nilijaribu kumfanya aje na kuhubiri kwa niaba yangu usiku wa leo, maana nilikuwa nimechoka sana, ama labda afanyize mstari wa maombi, a—akanikatalia, kwa hiyo, naye akasema, “Wakati mwingine, wakati mwingine.” Na—naye anaendelea kuniambia hivyo.

<sup>7</sup> Nami na—najua ya kwamba Ndugu Tommy Hicks ni, nimeninii, siku ambazo nimekuwa naye, na zile nyakati, na ushirika, bila shaka nina imani kubwa na Tommy Hicks, kwamba ni mtumishi wa Mungu aliye hai. Kipeo kikuu ambacho siamini kwamba kungekuwako na mtu yeyote angaliweza kusema lolote dhidi ya mwongozo wa Roho Mtakatifu kwa Ndugu Hicks. Kwa kuwa alikuwa tu. . . Siku moja wakati yeye. . . Mlisikia habari za ujumbe wake kwenda Ajentina, naye hata hakuwa na pesa za kwenda, lakini Bwana alimtuma, na, loo, mnajua kuhusu huo mkutano. Na mtu anayeweza kujitolea kwa Mungu namna hiyo!

<sup>8</sup> Mnajua, Mungu anaweza tu kutumia sehemu yako, unayoselimisha Kwake. Mnaona, kama nilivyosema, ninaamini, siku moja, mahali fulani, ninazungumza sana mahali mbalimbali, na asubuhi, na mikutano ya alasiri, na kadhalika, lakini nilisema hivi, ya kwamba Mungu anaweza kutumia kile unachosalimisha, kama vile Samsoni. Samsoni asingeusalimisha moyo wake kwa Mungu, huo alimpa Delila, bali alimpa Mungu nguvu zake, basi Mungu angeweza tu kutumia nguvu zake, hivyo tu.

<sup>9</sup> Lakini laiti jamaa mmoja angeweza tu kusalimisha utu wake wote kwa Mungu, sasa jambo ndilo hilo. Kama unaweza kuusalimisha mwili wa—wako, Mungu atautumia mwili wako. Kama unaweza kuisalimisha nia yako, moyo wako, chochote kile, Mungu atatumia kile unachompa kukitumikisha. Anatafuta kumpata mtu ambaye anaweza kumpata amejisalimisha namna hiyo.

<sup>10</sup> Mungu awe pamoja nawe, Ndugu Tommy, akupe mafanikio makubwa, makubwa mno. Tutakuombea katika ibada zako kule. Nami nitakuwa Canada, pia, katika siku chache, lakini huko juu upande wa pili, kwa hiyo. . . Akupe mafanikio makubwa na safari njema. [Ndugu Tommy Hicks anasema, “Mungu akubariki.”—Mh.] Sisi. . . Asante. Vivyo hivyo kwako, Ndugu Tommy.

<sup>11</sup> Tulikuwa na wakati mzuri asubuhi ya leo katika ushirika kwenye meza ya Mungu asubuhi ya leo kwenye, ambapo tuliomba baraka na tukapata kiamshakinywa cha wahudumu, mara ya kwanza niliyojaliwa kukutana na kundi la wahudumu wa jiji hili. Na bila shaka niliona baadhi ya watu mashuhuri, watumishi mashuhuri wa Kristo wenye mioyo hodari, wakimwendea Mungu.

<sup>12</sup> Nami ninatumaini ya kwamba tutaninii, wakati mwingine, tunaweza kurudi ambapo tuna mahali kamili, sote pamoja, na mkutano mkubwa wa ushirika na—na kuwa na mkutano mkubwa sote pamoja, hapa Chicago.

<sup>13</sup> Sasa, kulikuwako, jana jioni, nafikiri tulikuwa tukiwaombea wagonjwa. Na Jumapili alasiri, nilihubiri juu ya somo la *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*. Jana usiku, nilihubiri juu ya somo la *Taarifa Kubwa Sana Za Habari Zilizowahi Kuufikia Ulimwengu Katika Historia*.

<sup>14</sup> Na usiku wa leo, kama mtafungua Maandiko, mkipenda, kwenye Mathayo mlango wa 11 na kifungu cha 6, nitasoma maneno haya:

*Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami.*

<sup>15</sup> Nitaliita somo hili *Heri Iliyosahaulika*.

<sup>16</sup> Sote tunazifahamu zile Heri. Katika Ki—Kitabu cha Mathayo mlango wa 5, Yesu alifundisha hizo Heri alipochukua

watu na kupanda mlimani, kabla tu ya mwanzo, ama, wakati tu huduma Yake ilipoanza, Yeye akawa Kiongozi wao. Naye akapanda juu na kufundisha hizo Heri, na kuanza, “Mmesikia wakisema, watu wa kale, bali mimi nawaambia,” na kadhalika.

<sup>17</sup> Sasa, Yesu alikuwa ni mfano mkamilifu wa, ama, Musa alikuwa ni mfano wa Yesu; Yesu alikuwa Mfano wa Musa. Musa alikuwa na—nabii, alikuwa mtoa sheria, alikuwa kwa namna fulani kama mfalme juu ya hao watu huko nyikani, Israeli. Naye alizaliwa nabii, alifichwa kutoka kwa Farao, kama tu vile Yesu alivyofichwa kutoka kwa Milki ya Kirumi, naye, huduma yake na maisha yake yalifanana tu moja kwa moja. Naye Musa, alipowapeleka wana wa Israeli nyikani, alipanda katika, mlimani na kuchukua zile amri, akashuka na kuanza kufundisha zile amri.

<sup>18</sup> Naye Yesu, alipoingia katika mamlaka Yake, alipanda mlimani akaketi chini na kuanza kuwafundisha watu, “Heri wenye moyo safi, watamwona Mungu. Heri walio maskini wa roho, Ufalme wa Mungu ni wao. Heri ninyi mnapotukanwa, na kuteswa, na kudhihakiwa, na kadhalika, kwa maana waliwaudhi manabii waliokuwa kabla yenu. Furahini na kushangilia sana, maana thawabu yenu ni kubwa Mbinguni.”

<sup>19</sup> Alikuwa akimfananisha Musa hasa, ama, mfano wa Musa ulikuwa ni mfano Wake. Nasi sote tunafahamu mifano hiyo ya kile Musa alichokuwa na kile Yesu alichokuwa, akifundisha hizo Heri. Lakini Heri hii iko katika mlango wa 11 na kifungu cha 6, na usipoangalia, utairuka moja kwa moja wala hutaipata. Imebaniwa katikati ya maneno mengine, bali ni Heri. Naye akasema, “Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami.” Mnaona?

<sup>20</sup> “Heri wenye moyo safi... Heri wapatanishi... Heri... Heri...” Na huku mbali sana, Yeye anapenyeza Heri hii tena, mnaona, “Heri... Na, heri awaye yote, asiyechukizwa Nami.” Loo, ulikuwa ni wakati mzuri sana, katika siku hizo.

<sup>21</sup> Sasa, tunaona ya kwamba kilichosababisha jambo hili kuanza, ilikuwa tu ni baada ya huduma ya huyu Eliya mkuu, mgumu, wa Agano Jipya, Yohana Mbatizaji. Na hao ndio walipelekewa Ujumbe. Naye Yohana alikuwa amewekwa gerezeni kwa sababu ya huduma yake. Na loo, jinsi Yohana alivyokuwa jamaa mgumu! Naye kwa kweli alikuwa, kabisa, “yule mjumbe” Yesu alisema, “atakayenitangulia.” Naye alikuwa mtu wa porini.

<sup>22</sup> Na jinsi, walipomshika, alikuwa kama Eliya kikamilifu, ambaye roho yake ilitiwa mafuta, alikuwa ni Eliya aliyetiwa mafuta wa Agano Jipya. Jinsi ambavyo Eliya alikuwa m—mtu ambaye hakupendezwa na jinsi Yezebeli, wanawake watovu wa uadilifu, walivyoishi, naye Yohana, jambo lile lile; naye Eliya aliishi nyikani, Yohana, jambo lile lile; Yohana kwa namna fulani alikuwa msimama peke yake, kama vile tu Eliya alivyofanya.

Na mtu huyo mashuhuri, mshupavu kutoka nyikani, halafu basi wakamfunga kwenye maskini gereza lenye uvundo, lenye majimaji, lililolowana.

<sup>23</sup> Hilo hapana shaka lilikuwa tukio la kutisha sana kwa Yohana, mtu aliyekuwa huru, huko nje nyikani, akila chakula chake cha nzige, na asali, na safari ya nyikani, huko nje ambako angeweza kuua alichokula, ama kuchukua alichotaka kutoka nyikani, na sasa yuko chini katika maskini gereza chafu, lenye uvundo, labda lenye giza, kwenye shimo mahali fulani, kwa sababu mke huyo, Yezebeli, wa, Herodia alikuwa amemfanya atupwe mle ndani kwa sababu alikuwa amemwambia kwamba haikuwa halali kwake kumchukua, Herode, kumchukua mke wa ndugu yake Filipino, na kuishi naye, haikuwa halali kwake kufanya hivyo.

<sup>24</sup> Naye Yohana alikuwa mmoja wa wale watu ambao hawakusita kushambulia, alimwacha tu ashikwe na hamaki, haikuleta tofauti yoyote kwake, kama ilikuwa ni kukatwa kichwa, ilikuwa ni kukatwa kichwa, hivyo tu. Kama tu vile Eliya, yaliyompasa kusema aliyasema kinaganaga, yaliyo kweli, yalikuwa ni kweli, kama ilikuwa ni makosa, ilikuwa ni makosa.

<sup>25</sup> Mungu, tunahitaji wengi zaidi kama hao leo hii, watu watakosimama juu ya imani halisi ya kweli ya Neno la Mungu. Linene na usinyamaze, linene.

<sup>26</sup> Halafu tunaona hapo ya kwamba Yohana, huko chini katika maskini gereza chafu, lenye uvundo, pamoja na mikate michafu labda wangemtupia mara moja moja, labda alikuwa amekonda, wala hana njia ya kuisoma Biblia yake, naye angeninii, kidogo akashikwa na, ninii yake, kama vile mwandishi mmoja alivyoandika juu yake wakati mmoja, kasema, “Jicho lake la tai liliingia utando.”

<sup>27</sup> Mnajua manabii wanafananishwa na tai, naye Mungu huwaita manabii Wake tai. Ni kwa sababu tai ndiye mwenye nguvu kuliko ndege wote. Naye tai anaweza kwenda juu zaidi, kupaa juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote, naye ana jicho bora kuliko ndege mwingine yeyote.

<sup>28</sup> Wanzungumza juu ya mwewe kuwa na jicho, ama, na mwewe kuwa na uwezo wa kuruka juu hewani, mbona, kama mwewe angejaribu kumfuata tai, angechanganuka hewani, hakika angechanganuka. Na sasa, itamfaa nini tai kupaa kule kama hana *jicho* la kutosha kuona, mahali ambapo, kurudi chini duniani tena?

<sup>29</sup> Ni kama tu ikiwa, tunafanya nini kuruka juu kama hatujui tunarukia nini? Mnaona? Pia tunashuhudia nini sana, au kupiga kelele nyingi kama hatuna kitu cha kupigia kelele? Mnaona? Na ni tofauti sasa, kelele ni sawa kama una kitu cha kupigia kelele, lakini subiri mpaka hicho kije kwanza, ndipo itakuwa ni kelele maishani mwako mwote basi.

<sup>30</sup> Lakini tunaona ya kwamba jicho hili la tai lilikuwa limeingia utando, kwa sababu walikuwa wamemtoa katika makao yake nyikani, nao walikuwa wamemweka kwenye maskini gereza chafu, lenye uvundo, na mtu huyu mashuhuri ambaye angeweza kuwa tai wa kupaa juu hewani.

<sup>31</sup> Sasa, kadiri unavyopanda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Wanapaa juu sasa katika haya maputo na kadhalika, ili waweze, juu sana hewani, hata wanaweza kupiga picha ya dunia nzima, katika mpindiko wake. Nami nadhani, katika kifaa hiki kipya ambacho Urusi inacho, wanaweza kuuzunguka ulimwengu katika yapata saa moja na dakika arobaini na tano, mbona, wanaweza kufanya sinema yake yote ikizunguka. Lakini, kadiri unavyopaa juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi.

<sup>32</sup> Kwa hiyo, manabii katika Biblia, walikuwa ni wale tai ambao wangeweza kupaa juu *sana* na juu ya kusanyiko, na kuona BWANA ASEMA HIVI ilikuwa ni nini, kisha warudi chini na kuleta habari. Mnaona? Kwa hiyo Neno la Bwana liliwajia manabii. Basi Yohana akiwa amefungiwa kizimbani, mbona, ilitia utando jicho hilo la tai.

<sup>33</sup> Nilimsikitikia sana, tai mkubwa, wakati mmoja. Nami siwezi kuvumilia kwenda kwenye bustani la wanyama, kuwaona maskini hao jamaa wamefungiwa kizimbani, akina simba, na, jinsi tu wamefungwa kifungo cha maisha. Basi mimi na mtoto Sarah, wakati mmoja, kwenye Bustani ya wanyama ya Cincinnati, hapa, tulikuwa tukitembea huku na huku, naye mama alikuwa akiandaa chakula chetu cha kutwa. Tulikuwa huko juu pamoja na watoto, huko juu, wanapenda kuendesha mashua ndogo na kuwaona tumbili na kadhalika. Kwa hiyo tulikuwa tukitembea huku na huku mama alipokuwa akiandaa chakula cha kutwa.

<sup>34</sup> Ndipo nikasikia kelele, nami nikashuka chini ya kilima kuona ilikuwa ni nini. Nao walikuwa ndio kwanza wamkamate tai mkubwa na walikuwa wamemweka kizimbani. Ndipo nikamwanguka maskini jamaa huyo pale, naye alikuwa akitokwa damu kichwani mwake mwote, nayo manyoya yalikuwa yameng'olewa kichwani mwake na kwenye ncha za mbawa zake. Nami nikamwanguka huyo jamaa mkubwa akitembea pale, ndipo huyu hapa angekuja, akijaribu kuruka, kama tai afanyavyo. Naye angegongesha kichwa chake kwenye nguzo hizo, zikamrusa nyuma kichalichali, akaanguka sakafuni, na kulala hapo na kufingirisha macho hayo makubwa, na kuangalia juu namna *hiyo*. Kisha arudi tena, naye huyu hapa angekuja na kugonga nguzo hizo tena, na damu na manyoya yakamtoka, naye angelala chali, afingirishesha macho hayo makubwa na kuangalia juu.

<sup>35</sup> Kwa nini? Alikuwa ni ndege wa kimbinguni, alikuwa

akiangalia juu mahali anapapaswa kuwa. Lakini hila fulani za ujanja wa mwanadamu zilikuwa zimemweka kizimbani. Nami nilifikiri hilo lilikuwa tamasha la kuchukiza sana, la kusikitisha. Ningelimnunua tai huyo kama ingalinilazimu—kama ingalinilazimu kuchukua sadaka yangu ya kwanza kumnunua huyo tai, kumwachilia.

<sup>36</sup> Nikawaza, “Maskini jamaa huyo,” nikawaza, “jamani, kama hilo si baya sana, ambaye, alizaliwa kuwa ndege wa kuruka angani, naye huyu hapa kwa hila za wanadamu, amefungiwa kizimbani kabisa, naye anaugongesha tu ubongo wake, lakini amefungiwa kizimbani.” Nikawazia, “Hilo ndilo tamasha la kuchukiza sana nililopata kuona.”

<sup>37</sup> Ndipo nikageuka niondoke, nami nikawazia, “Naam, hilo ni tamasha la kuchukiza, lakini nimeona kitu cha kuchukiza kuliko hicho, kuona wanaume na wanawake waliozaliwa kuwa wana na binti za Mungu wamefungiwa katika kizimba cha namna fulani, wakati basi wanapoangalia juu na kujua kuna Mungu wa Mbinguni, kujua ya kwamba Yeye ni Mponyaji mkuu, na Mwalimu mkuu, na Mwokozi mkuu, na halafu wamefungiwa katika namna fulani ya kizimba cha kikanisa, ambapo wanagongesha tu bongo zao kwa mashirika ya kila namna, na chochote kile, na kamwe wasiweze kutoka nje ya hicho kizimba.”

<sup>38</sup> Hiyo ni hali ya kusikitisha. Wanaambiwa juu ya Mungu mkuu aliyekuwako, na kuwajenga chini ya matarajio, kisha wanakibomoa kitu hicho chote kutoka chini yao, “Yeye alikufa na kuwekwa kaburini na hamna lingine, Yeye si kama alivyokuwa.” Hilo ni tamasha la kusikitisha, kuona watu, wanaume kwa wanawake waliozaliwa wapate kuwa watoto wa Mungu na kufungiwa katika vitu kama hivyo.

<sup>39</sup> Yohana, jicho lake la tai kweli lilikuwa limeingia utando. Naye Yohana alikuwa amechoka. Yeye na Eliya walikuwa wanafanana sana, kwa sababu roho yule yule alikuwa juu ya, huyu, mtu mwingine. Mnaona, Mungu kamwe haichukui roho yake, Yeye humchukua tu mtu Wake. Mungu alimchukua Eliya, akaichukua roho ya Eliya na kuiweka juu ya Elisha, kisha akaiondoa kwa Elisha, na kuiweka juu ya Yohana, kisha akaahidi kuiweka tena katika wakati wa mwisho, mtu mwingine atakayekuja wakati wa mwisho, Eliya mwingine. Ambalo sisi sote, kama wasomaji wa Biblia, tunajua ya kwamba tumeahidiwa hilo.

<sup>40</sup> Sasa, tunaona, basi, ya kwamba ibilisi humchukua mtu wake bali kamwe si roho yake, naye anaendelea tu kushuka moja kwa moja vivyo hivyo. Nasi tunaona ya kwamba hao wawili wako pamoja.

<sup>41</sup> Nasi tunaona ya kwamba—ya kwamba Eliya na Yohana walikuwa wanafanana sana. Walikuwa watu wenye wasiwasi

sana, wote wawili karibu washikwe na mfadhaiko, wote wawili. Na watu wanaoishi karibu na Mungu mara nyingi huhesabiwa kuwa ni waliochanganyikiwa ama wana kasoro. Hiyo ni kweli, daima wanadhaniwa hivyo.

<sup>42</sup> Paulo, asubuhi ya leo, nilipokuwa nikizungumza na kundi la wahudumu, Agripa alimwambia, ama, Festo alisema, “Kusoma kupita kiasi kunakufanya mwendawazimu, ama mwenye kichaa.”

Akasema, “Sina wazimu, sina kichaa, nina akili timamu.” Mnaona? “Na mimi—mimi niko sawa.”

<sup>43</sup> Na kwa, wanadai, kama vile William Cowper, naamini ndivyo ilivyokuwa, niliposimama kwenye kaburi lake kule London, naye aliandika ule wimbo maarufu:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,  
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,  
Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini  
ya hilo gharika,  
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

<sup>44</sup> Mtu huyo alivuviwa sana hata yeye, baadaye, akajaribu kuchukua kamba na kujinyonga, hiyo kamba ikakatika. Alijaribu kwenda mtoni kujiua, nayo tekisi hata haikuweza kuuona huo mto, kulikuwa na ukungu sana.

<sup>45</sup> Na ili kuonyesha tu jinsi ambavyo uvuvio huo humshika mtu, unamnyakua, basi atakapotoka kwenye huo, kama vile Stephen Foster, aliyelipa taifa hili nyimbo zake kuu sana za jadi, *Mzee Mweusi Joe, Chini Kwenye Mto Swanee, Makazi Ya Kale Ya Kentucky*, kila wakati ambapo angepata uvuvio na kuandika wimbo, basi angeingia ulevini, hatimaye, akaingia chini ya, akatoka kwenye huo uvuvio, akamwita mtumishi na kuchukua wembe akajia.

<sup>46</sup> Kisha ninawazia juu ya nabii Yona, Mungu akimvuvia yule tai mkuu kwa ajili ya hewa ya siku hiyo. Mungu alimvuvia sana, mpaka akashuka akaenda kule na kulala katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, akatembea ukingoni na kutoa ujumbe ambao uliwafanya hata hao watu kuwavalisha wanyama wao nguo za magunia. Ndipo Roho alipomwacha, alipanda juu ya kilima, akaketi chini na kumwomba Mungu amwache afe. Hiyo ni kweli.

<sup>47</sup> Tunamwona huyu Eliya mkuu, ambaye Yohana alikuwa mfano wake, yule tai mkuu wa siku hiyo, mtu mwenye nguvu, mgumu, mtu mkubwa wa mwituni, aliishi mwituni katika pango, naye akatoka, akaja miongoni mwa watu kwa kishindo, naye Mungu angempandisha juu mahali ambapo Israeli hawakujua lolote kupahusu, na kutangaza ujumbe na kusema, “Ni BWANA ASEMA HIVI,” kisha arudi nyikani kwa kishindo tena.

48 Kuona tai huyo mkuu, wakati alipotoka kule kwa kishindo na kumwambia mfalme huyo, “Hata hakutakuwa na umande kutoka mbinguni, ila kwa neno langu.” Akarudi moja kwa moja huko nje, wakati aliposhuka kwenye barabara hiyo ya Samaria siku hiyo, fimbo hiyo mkononi mwake, amejifunga kipande hicho cha ngozi ya kondoo, kichwa hicho chenye upara kiking’aa, masharubu yakining’inia chini, hatua hizo imara kadiri zilivyoweza, zikishuka kwenye barabara hiyo ya Samaria.

49 Lakini alijua alikuwa Mbele za Nani. Hakuogopa yale Ahabu aliyokuwa anataka kusema, kwa sababu alikuwa Mbele ya Mtu fulani aliye mkuu kuliko Ahabu. Alikuwa kwenye huo Uwepo, naye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Maskini macho hayo, yakiwa huko nyuma, pamoja na yale makunyanzi, yalikuwa yakiangalia moja kwa moja angani, alikuwa akitembea imara, kwa sababu alijua alikuwa na BWANA ASEMA HIVI.

50 Loo, alikuwa ni tai. Akapanda juu ya mlima, akanywea kwenye kijito huko mpaka kikakauka, kisha akarudi kule chini na kuitisha m—mkutano, wakati Mungu alipompa ono, akapanda juu ya mlima, na kusema, “Hebu na tuthibitisha Mungu ni nani. Hebu tuone Mungu ni nani. Kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu.” Hiyo ni kweli. Loo, ninawapenda hao tai. Naam, bwana.

51 Akapanda akaenda kule na kusema, “Kama Yeye. . . Hebu tumthibitisha Mungu,” naye akasema, akakumbuka vile Mungu alivyomwambia lile ono, akasema, “ninyi mchukueni fahali, na—nami nitamchukua fahali, kisha mumwite Baalimu, nami nitamwita Mungu, na yeyote yule atakayejibu kwa Moto, Huyo na awe Mungu.”

52 Na wakati alipokuwa na hakika sana kwa nafsi yake, hakika sana na ono lake, wakati walipokuwa wakimwita Baalimu asubuhi yote na kujikatakata, na kupiga mayowe, na kurukaruka, akatembea huku na huku, kasema, “Aisee, labda afadhali mpige mayowe zaidi kidogo, labda amesafiri, ama labda amelala kidogo.” Mnaona? Loo, alijua mahali alipokuwa amesimama. Ilikuwa hivyo!

53 Lakini baada ya kumthibitisha Mungu, jicho lake la tai lilitiwa utando, ndipo wakati Yezebeli alipotishia ya kwamba angemwua, yeye alikimbilia nyikani. Mungu alimkuta mtumishi Wake amelala chini ya mretemu, akikimbia, baada ya kumthibitisha Mungu kuwa ni Mungu.

54 Wasiwasi, fadhaa, unapopanda juu katika milki hizo, inaufanyia jambo fulani moyo wa mwanadamu. Unaposhuka, hu—huwezi kulielezea, inakupeleka mahali fulani, hakuna haja ya kujaribu kulizungumzia. Maono na kadhalika yanayokururua vipande—vipande, huwezi kuwaambia watu wengine, hawaelewi. Hawajawahi kuwa kule, kwa hiyo ungejua je habari zake? Kwa hiyo, inawararua vipande—vipande.



<sup>55</sup> Mungu, ni mwema sana kwa mtumishi Wake, hata hivyo, kumlisha na kumtia moyo, na huko nje chini ya mretemu. Lakini baada ya kuwa na imani kubwa hivyo katika Yehova, akiwa na *hakika* sana, hata angeweza kwenda mbele ya mfalme, na kusema, “Hata umande hautaanguka, ila kwa neno langu.” Akatoka kwa kishindo moja kwa moja kwenye jumba la mfalme, ametiwa mafuta.

<sup>56</sup> Ndipo akawa na ono la jambo la kufanya. Ndipo akatoka moja kwa moja huko kwenye mlima huo na kuchukua, na kuagiza Moto ushuke kutoka mbinguni, akithibitisha Yeye alikuwa ni Mungu, kisha akaagiza mvua inyeshe kutoka mbinguni siku ile ile, kisha akaua watu mia nne, makuhani, makuhani wapagani, akakata vichwa vyao, kisha akatoroka wakati hilo ono lilipomwacha.

<sup>57</sup> Mwenye wasiwasi, ameketi pale nje, kasema, “Mimi si bora kuliko baba zangu wengine. Mimi si zaidi ya hao manabii wengine. Sasa, Bwana, chukua uhai wangu, Mimi ndiye pekee niliyesalia, mimi pekee ndiye ninayehubiri Injili ya kweli, kwa hiyo utwae tu uhai wangu, niache niende.” Wote wanafadhaika sana namna hiyo.

<sup>58</sup> Lakini Mungu akasema, “La, ni—ni—nina—nina elfu saba wengine, ambao hawakuwahi kumpigia Baalimu goti bado.” Mnaona? Mnaona? “Lakini mimi, hiyo ni sawa Eliya, unafanya kazi kubwa, bali ni—ningali nina kundi lingine,” mnaona, “ambalo hulijui bado.”

“Lakini utwae uhai wangu. Mimi si zaidi ya baba zangu walivyokuwa, manabii walionitangulia. Acha nife.”

<sup>59</sup> Na hapa, Yohana, zaidi sana kama yeye, amelala hapa chini gerezani, akijipa moyo, akiisha kusimama ukingoni mwa Yordani, akatoka nyikani, akampokea Roho Mtakatifu katika tumbo la mama yake, miezi mitatu kabla hajazaliwa. Hakika alimpokea.

<sup>60</sup> Jinsi gani? Aliposikia Jina la Yesu Kristo kwa mara ya kwanza, wakati Mariamu alipopanda kule, naye alikuwa, hajapata bado, kamwe hakuwa amehisi chochote, yule Malaika alikuwa ndiyo kwanza amtie uvuli, Roho Mtakatifu alikuwa amemwambia. Akaondoka akaenda Uyahudi, naye alikuwa, uh, akamwambia Elisabeti, ya kwamba alikuwa na mimba, naye kasema, “Mungu amenitia uvuli, nami nitapata Mtoto, na akasema nitamwita Jina Lake Yesu.”

Naye mtoto Yohana alikuwa na miezi sita, tayari, Elisabeti alikuwa, katika umama wake, uja uzito, naye alikuwa bado hata hajahisi uhai.

<sup>61</sup> Na kwa hiyo wakati alipokuwa amesimama, akiutazama uso wa Mariamu, huku Mariamu akimwambia yale Roho Mtakatifu aliyosema yangetukia (Naye alikuwa amemwelezea tukio alilokuwa nalo, mwanamke mkongwe alikuwa amechukua

mimba, na halafu jinsi mumewe alivyofanywa bubu.), basi akiwa amesimama pale, ndipo yeye akasema, “Ni—nitamzaa Mwana na kumwita Jina Lake Yesu,” na mara hilo Jina la thamani na tukufu la Yesu lilipotamkwa kwa mara ya kwanza katika mdomo wa mwanadamu, maskini mtoto mchanga aliyekufa, amelala tumboni mwake, akaruka, akawa hai, na kumpokea Roho Mtakatifu, katika tumbo la uzazi la mama.

<sup>62</sup> Kasema, “Mama wa Bwana wangu amenijiliaje? Maana mara sauti ya kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto changu kichanga kiliruka kwa shangwe tumboni.” Nayo Biblia ilisema alizaliwa amejaa Roho Mtakatifu tangu tumboni mwa mama yake.

<sup>63</sup> Mtu aliyetitwa na Mungu, aliondoka akaenda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa, hana elimu, akaenda nyikani naye alikuwa mtu wa mwituni.

<sup>64</sup> Akiwa na umri wa miaka thelathini, alitoka nyikani akihubiri Ujumbe mzuri sana wa Masihi ajaye, hata akayatikisa hayo maeneo. Wala hakuogopa mafundisho ya Mafarisayo, kasema—kasema, “Enyi nyoka nyasini, msije huku mkisema, ‘Tunaye Ibrahimu baba yetu.’ Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo?” Loo, jamani. Alikuwa mkali.

<sup>65</sup> Kasema, “Ninawaambia juu ya Masihi ajaye na pepeto mkononi Mwake,” amina, “Atausafisha sana uwanda Wake, atapeleka ngano Yake ghalani, na makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.” Whiu! Alijua alichokuwa akizungumzia.

<sup>66</sup> Sasa, lakini wakati Masihi huyu hatimaye alipokuja, wakati Masihi hatimaye alipokuja, naye Yohana alikuwa na heshima ya kumbatiza, alikuja vi—vizuri kabisa, ishara zote zilikuwa sahihi, alionyesha ishara ya Masihi, naye Yohana alijua hilo, kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, huyo ndiye Masihi, hapana shaka juu yake. Yohana alisema, “Niliona ile Nguzo ya Moto, Nuru ikishuka juu Yake katika mfano wa hua, Sauti ikinena kutoka kwenye hiyo Nguzo ya Nuru, ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake.’”

<sup>67</sup> Alijua huyo alikuwa ni Masihi, Yohana akasema, “Sikumjua Yeye, bali Yeye, alikuwa nyikani, aliniambia niende nikabatize kwa maji, kasema, ‘Yule utakayemwona Roho akimshukia na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.’ Nami nina hakika Huyu Ndiye.” Kwa hiyo akaitangaza kwa nguvu kabisa.

<sup>68</sup> Lakini shida ilipoingia, Yesu alikuwa na kumwonyesha Masihi, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, lakini basi jambo fulani likaenda kombo. Yohana alikuwa amemtambulisha Masihi akiwa na pepeto mkononi Mwake, akienda kuyateketeza makapi. Lakini aliona kazi za Yesu, Yeye alikuwa mpole na mnyenyekevu. Kwa hiyo ikamtia wasiwasi. Hakujuu—hakujuu la

kusema. A—akawazia, “Sasa, kuna kasoro hapa mahali fulani.” Ilionekana alikuwa—alikuwa ameamini jambo baya, ilionekana kana kwamba halikuwa likitenda kazi vizuri.

<sup>69</sup> Na kuna mara nyingi ambapo tunafikiri, pia, ya kwamba halifanyi kazi vizuri. Lakini linafanya kazi vizuri. Mradi tu tunajua ya kwamba Yeye yupo hapa, inaleta tofauti gani? Linafanya kazi vizuri. Labda halifanyi kazi sawasawa na vile tunavyodhani linapaswa kufanya kazi, bali linatenda kazi sawasawa na vile Mungu anavyotaka litende kazi.

<sup>70</sup> Unasema, “Vema . . .” Yohana aliwazia, “Vema, sasa, nilimtambulisha Masihi aliyekuwa na pepeto Lake mkononi Mwake, Naye alikuwa anaenda kusafisha sakafu, na kuipeleka ngano Yake ghalani. Nami nikawaambia ya kwamba shoka lilikuwa limewekwa kwenye shina la mti, Naye alikuwa anaenda kuchukua takataka zote na kuziteketeza. Naye Huyu hapa, badala ya Mtu mashuhuri, mwenye nguvu kama huyo, Huyu hapa anakuja mpole na mnyenyekevu. Hapana shaka kitu fulani kilienda kombo mahali fulani,” akasema, “hapana shaka ila kuna kasoro mahali fulani.” Alidhani haikuwa sawa.

<sup>71</sup> Alifadhaika kama wengi wetu tunavyofadhaika. Tunapooni mambo yakiendelea ambayo si yale tunayofikiri ni sawa kabisa, tunafadhaika. Usisumbuke, itakuwa sawa.

<sup>72</sup> Ibilisi alimshika mle ndani, ibilisi akawazia, “Sasa, nimemtia gerezani sasa, nimemtupa gerezani, kwa hiyo nitamvuruga kabisa wakati nikiwa nimemweka mle. Mungu hamtumii sasa hivi, nimemtia gerezani, kwa hiyo nitaweka tu kila namna ya blanketi juu yake niwezayo. Nilimfungia kizimbani kabisa, nimemweka tai kizimbani, kwa hiyo nita—nitaninii tu—nitamfanya tu ajutie kuihubiri Injili.”

<sup>73</sup> Hivyo ndivyo anavyowafanya *wengi*. Na kuna watu wengi wazuri katika hali ile ile siku hizi. Hiyo ni kweli kabisa. Tunafikiri haifanyi kazi vizuri, lakini inafanya kazi vizuri, kila kitu ni sawa.

<sup>74</sup> Hapa hivi majuzi, maskini . . . Mimi huwaona watu wengi sana wanaoingia, kasema, “Vema Ndugu Branham, niliombewa kwa ajili ya . . . Ha—ha—hakika sikuona tofauti yoyote, vema, kuna kasoro.” La, hakuna. Huo mfumo hauna shida yoyote, Mungu hana shida yoyote, Biblia haina shida yoyote, Roho Mtakatifu hana shida yoyote, jambo ni kwamba, una shida *wewe*.

<sup>75</sup> Kila kitu kilikuwa kikienda sawa, ilikuwa ni Yohana tu. Hivyo tu.

<sup>76</sup> Kwa hiyo kulikuwa na mama aliyeshuka hivi majuzi kutoka—kutoka Mji wa Zion, huenda akawa hapa sasa, yapata mwezi mmoja uliopita. Maskini mwanamke huyo, maskini mume wake, maskini mume na mke wa kupendeza, basi walikuja nyumbani kwangu, na—nao wakashuka pamoja na marafiki

zangu wazuri, akina Simses, kutoka huko Zion. Na huenda wote wameketi hapa usiku wa leo ni juavyo mimi.

<sup>77</sup> Naye alikuwa na mtoto mchanga, nafikiri alizaliwa huku mguu wake ukining'inia *hivi* na—na asingeweza kuushusha mguu wake. Ndi—ndipo akasema tu, “Kama ninaweza tu kumwona Ndugu Branham akiweka mikono yake juu ya mtoto huyu mchanga, mguu huo utashuka chini.” Mbona, alimletea viatu vya kuvaa nyumbani na kadhalika. Naye, huyo ni, “Naam, bwana.”

<sup>78</sup> Kwa hiyo nilikuwa nikiomba huko maskanini kwenye, ama, nikihubiri, ndipo basi nilipomaliza, nilikuwa nikijaribu, kupata njia ya kwenda kwenye mkutano mwingine na, ama, huko Bloomington, Illinois, ndipo basi, muda si muda mwajua, nilipoanza kuondoka jukwaani, ninaamini tulikuwa tukiingia, Kutawadhana miguu.

<sup>79</sup> Sisi, tunaamini katika Kutawadhana miguu, na—naamini hiyo ni, Biblia inafundisha hiyo, nasi tunapaswa kufanya hivyo mpaka Yeye atakapokuja, na kwa hiyo tunajaribu kutimiza kila Neno alilosema. Nasi tulikuwa tukiadhimisha jambo hili kanisani mwetu, jambo ambalo tumefanya sikuzote, kwa miaka thelathini sasa.

<sup>80</sup> Tulikuwa tukienda Kutawadhana miguu, ndipo—ndipo mwanangu akaja, na kusema, “Baba, kuna—kuna watu waliotoka Zion pale,” kasema, “walikuwa wakitarajia kuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa usiku wa leo,” akasema, “wana mtoto mchanga ambaye, mwanamke huyo anaamini kama ukimwomba mtoto huyo mchanga, huo mguu mdogo ungeshuka chini, ana mguu mbaya.”

Nikasema, “Mlete hapa.”

<sup>81</sup> Ndipo maskini huyo mama mdogo, mrembo, akaja na kusema, “Mtoto wangu mchanga, Ndugu Branham, tumeamini, mimi na mume wangu, utakapoweka mikono yako juu ya mtoto huyu mchanga, kwamba mguu utanyooka, utakuwa sawa.”

Nikasema, “Je, unataka nipate ono kutoka kwa Bwana?”

Akasema, “La, bwana, mwekee tu mikono yako.”

Nikasema, “Vema, nitafanya hivyo.” Nikaweka mikono yangu juu yake, nikamwomba, nikaingia chumbani.

<sup>82</sup> Basi kesho yake nilikuwa huko nje ofisini. Nilipokuwa nimeketi huko nje na—na kujibu simu, na—na kufanya kazi fulani pale ofisini, gari moja likaja, ndipo maskini mama huyo akatoka, yeye, na mumewe, nao hawa hapa wakaja, kasema, “Ndugu Branham,” kasema—kasema, “jambo fulani lilienda kombo.”

Nikasema, “Loo, vema, unamaanisha nini?”

“Mbona,” akasema, “m—mguu wa mtoto huyo bado haujashuka.”

Nami nikasema, “Vema, hilo lina uhusiano gani nalo?”

<sup>83</sup> Naye akasema, “Vema, ni—ni—niliamini, Ndugu Branham, Niliamini ikiwa tu ungemwekea mikono mtoto wangu mchanga ya kwamba Mungu angemponya.” Kasema, “Niliamini.” Kisha kasema, “Kitu fulani kilienda kombo mahali fulani.” Akasema, “Labda afadhali upate ono kwa ajili yake.”

Nikasema, “La. La. Hakuna kitu kibaya, la, hakuna hata kitu kimoja kibaya, kitu kibaya tu ni wewe.” Mnaona? Nikasema, “Wewe amini tu.”

Akasema, “Nitauliza jambo moja: Ndugu Branham, unafikiri ni mapenzi ya Mungu mtoto wangu awe kiwete?”

Nikasema, “Siamini ni mapenzi ya Mungu.”

<sup>84</sup> Yeye, “Hayo ndiyo yote niliyotaka useme.” Kutoka hapo akaenda. Na siku chache zilizopita walipiga simu, na sasa, mguu wa mtoto umerudi kawaida, umeshuka. Wao. . . Mnaona, tunachanganyikiwa tu, hivyo tu, kila kitu kinakwenda sawa, kila kitu ni kulingana kabisa na wakati.

<sup>85</sup> Kwa hiyo tunaona hapa ya kwamba ibilisi hujaribu kuwafanya watu waamini, ama, wasiamini. Kwa hiyo ibilisi alikuwa akijaribu kumfanya Yohana asiamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Kwa hiyo akawakusanya wawili kati ya wanafunzi wake, naye akawatuma, kasema, “Sasa, ninyi nendeni mkatafute popote Yeye anapohubiria, na mtakapompata, nendeni mkamwulize, ‘Je, nimekuwa makosani?’” Mngeweza kuwazia hilo?

<sup>86</sup> “Je, ninaweza—ninaweza—ninaweza kuwa nimekosea? Yeye kweli ni Yeye yule? Najua ile ishara ilikuwa sahihi, niliona ile ishara ya Masihi, nilijua hiyo ilikuwa ni kweli, lakini—lakini huyu *mpole na mnyenyekevu*, na yote *haya*, si—silipati, haininii. . . Siwezi kulielewa, siwezi kuling’amua, silifahamu.”

<sup>87</sup> Hupaswi kulielewa. Kama ningeweza kukwambia jambo lote, nawe ulijua yote, nami nilijua yote, haingekuwa imani tena. Chochote ninachoweza kuelezea kikamilifu si imani tena. Kwa *imani* umeokolewa. Kwa *imani* umeponywa. Liamini tu. Huwezi kulielezea, liamini tu.

<sup>88</sup> Kwa hiyo akasema, “Nendeni, mkamwulize Yohana, ama, mwulizeni, kama tumtazamie mwingine. Je ninii yangu, imani yangu, matumaini yangu na ninii ya—yangu yalikuwa. . . Niliona ishara hiyo ya Masihi juu Yake, kwani—kwani nimekosea? Ni—nimechanganyikiwa? Sasa, kuna kitu kimeenda kombo?”

<sup>89</sup> Sasa, wanafunzi hawa walipomjia Yesu wakiwa na ujumbe wa nabii huyu mkuu, Yesu kamwe hakuwaambia, “Sasa, nitawaambia nitakalofanya, nitawatumia vitabu kadhaa mkampe Yohana: *Jinsi Ya Kuwa Na Furaha Gerezani*.” La,

Yeye—Yeye kamwe hakusema hivyo. Hakuninii—Hakusema, “Nita—nitawapa kitabu juu ya subira, nanyi mkamwambie Yohana jinsi ya kuwa na subira wakati akiwa gerezani. Ni—ni jambo jema, yuko gerezani, nami nachukia, kumwona gerezani, lakini nitamwambia jinsi—jinsi ya kufanya jambo hilo, loo, kuwa tu na furaha.”

<sup>90</sup> La, Yeye kamwe hakusema hivyo. Mnajua yale aliyosema? Alisema, “Kaeni tu mpaka mkutano wa alasiri ya leo. Kaeni tu huku, ndipo mnaweza kuondoka baada ya hapo. Angalieni tu mkutano wa alasiri ya leo.”

<sup>91</sup> Na baada ya Yesu kufanya huo mkutano... Ningewazia hao wanafunzi wa Yohana, wameketi pale, wakiangalia kila hatua aliyofanya, maana Yohana alikuwa amewafundisha kile Masihi huyo alichokuwa, na kuwaambia ilikuwa ni nini, na hawa walikuwa ni wanafunzi wake. Nao wakaanza kuona kile kilichotukia.

<sup>92</sup> Kwa hiyo basi baada ya ibada kwisha, ndipo hao wanafunzi wawili waliporudi kukutana na Yohana, Yeye akasema, “Enendeni, mkamwambie Yohana viwete wanatembea, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, na wote wanaokuja mkutanoni ni maskini. Na ma—maskini wote wamehubiriwa Injili. Kisha mumwambie Yohana asiogope, asiwazie chochote tofauti, niko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa, kila kitu kinaendelea sawa, kila kitu ni sawa. Niko kwenye wakati uliopangwa hasa. Nendeni, mkamwambie kuna ibada ya uponyaji inayoendelea, maskini wamehubiriwa Injili, nguvu za Mungu zinatenda kazi miongoni mwao. Niko kwenye wakati uliopangwa hasa. Msivutiwe na kitu kingine chochote. Niko kwenye wakati uliopangwa hasa.”

<sup>93</sup> Loo, jamani! “Na, heri yeye asiychukizwa Nami.” Sasa, usichukizwe. Ninaamini kuna watu wengi zaidi waliochukizwa na Yesu kuliko mtu mwingine yeyote aliyepata kuishi duniani, wanachukizwa upesi sana.

<sup>94</sup> Yesu sasa, katika heri hii isiyowekwa mahali pake, alinyemelea pale ili tuweze kuipata usiku wa leo, mbona, Yeye alisema, “Heri yule, asiychukizwa Nami. Msichukizwe Nami. Haidhuru ni jambo gani linalotukia, mimi niko, kila kitu kinafanya kazi sawasawa na wakati uliopangwa, kwa hiyo ne—nendeni tu mkaliamini, hivyo tu, kila kitu ni sawa. Endeeleni tu na kuliadini.”

<sup>95</sup> Mnajua, hapo, Yesu hakumkemea Yohana kwa jambo hilo. Yeye hakusema, “Vema, ninamwonea aibu mtume Wangu; ninamwonea aibu nabii Wangu.” La, kamwe hakusema hivyo. Hakusema, “Ulimwengu utasema nini kuhusu jambo hili, utakapokuja ukihubiri, ‘Loo, Masihi mkuu namna hiyo, na Masihi mkuu namna hiyo,’ halafu unatuma watu kuuliza kama Mimi ndiye Masihi?” Kamwe hakumkemea.

<sup>96</sup> Lakini wakati Yohana aliposema jambo baya kuliko yote ambalo angeweza kumwambia Yesu, Yesu alisema jambo zuri sana ambalo Yohana aliwahi kusema kumhusu. Naam.

Yesu... Yohana alisema, “Enendeni, mkaone kama Yeye Ndiye.”

<sup>97</sup> Ndipo wakiisha kuondoka, Yesu alisema, aliwaambia, Yeye alisema, baada ya wanafunzi wa Yohana kuondoka, alisema, “Mlitoka kwenda nyikani kuona nini? Mlitoka kwenda kumwona mtu aliyevaa ninii nzuri...?” La, alikuwa mbali sana na Hollywood kwa hilo. Kwa hiyo akasema, “Je, mlienda kumwona mtu aliyevaa mavazi mororo?” Kasema, “Wao ni wa ikulu za mfalme.” Akasema, “Mlienda kuona nini, u—u—unyasi ambao dthehebu lolote lingeweza kuupulizia vyovyote lilivyotaka?” Loo, la. Hakika sivyo.

<sup>98</sup> “Basi mlienda kuona nini? Nabii?” Kasema, “Naam, mlienda kumwona nabii, na aliye mkuu zaidi, yeye ni zaidi ya nabii.” Kasema, “Huyu ni yule Eliya, huyu ndiye yule aliyenenwa na nabii, ‘Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.’” Kasema, “Amin, nawaambieni, hapajawahi kuwa na mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama Yohana Mbatizaji.”

<sup>99</sup> Yeye hakumhukumu kamwe, Yeye alijua ya kwamba alikuwa ametiwa mafuta kwa roho ya Eliya, na roho huyo aliyekuwa juu yake, huyo ndiye aliyefanya hilo. Alijua kila kitu kilikuwa kikiendelea sawa, kila kitu kilikuwa kikiendelea sawasawa na wakati uliopangwa.

<sup>100</sup> Yohana, kwa nini yeye alikuwa mkuu kuliko—kuliko manabii wote? Sasa, kama wewe ni wa kiroho, utashika kitu fulani. Ni kwa nini yeye alikuwa mkuu kuliko wote? Manabii wengine wote walikuwa *wamenena* juu ya Masihi, lakini Yohana *alimtambulisha*, yeye ndiye *aliyemwasilisha*. Ndivyo itakavyokuwa katika wakati wa mwisho. Kila kitu kinaendelea sawasawa na wakati uliopangwa.

<sup>101</sup> Usichukizwe, amini tu. Siku hizi makanisa yamechukizwa Naye. Makanisa yamechukizwa, watu wamechukizwa, wote wamechanganyikiwa, hawajui la kuwazia, “Telepathia ya akili, kitu kingine, na yote...” La, usichukizwe.

<sup>102</sup> Ujumbe wetu Jumapili iliyopita ulikuwa ukijaribu kuwaonyesha yale Mungu aliyomfanyia Ibrahimu na kwa Uzao wake baada yake. Nasi tuliona, kwenye kila njia panda alimchukua Ibrahimu, akauchukua Uzao Wake, kuptia kuhesabiwa haki, kupitia kutakaswa, kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, kupitia kuwekwa kwa Mwana mahali pake, na ndipo Mungu akaja katika mwili wa kibinadamu, akageuza mgongo Wake kwenye hema la Sara, na kusema yale aliyokuwa akiwazia moyoni mwake.

<sup>103</sup> Usiogope, Yeye yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa. Um-hum. Yuko hapa! Usichukizwe Naye. “Heri

wao, wasiochukizwa Nami.” Angalikuwa hapa kuzungumza usiku wa leo, Yeye angesema jambo lile lile.

<sup>104</sup> Yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa. Nabii alisema kutakuwa na wakati ambao hautakuwa mchana wala usiku, lakini wakati wa jioni, itakuwa Nuru. Yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa.

<sup>105</sup> Tayari amepitia kuhesabiwa haki, Wakati wa Luther; utakaso, Wakati wa Wesley; Wakati wa Kipentekoste, tayari ameweka karama Zake kanisani; na sasa, akaonekana kwetu katika miili yetu kama vile Yesu alivyosema angefanya.

<sup>106</sup> Msichukizwe Naye, Yeye hajachelewa. “Ewe Yohana toka kwenye jela hiyo.” Ondoka kwenye dhehebu hilo lililoliamini. Ondoa pingu kutoka machoni mwako, wewe ni mtu huru kama utaamini. Yeye yuko kwenye wakati unaofaa kabisa. “Itakuwa nuru wakati wa jioni.” Amina.

<sup>107</sup> Nuru za jioni zinaangaza. Yeye ni nini? Yesu yule yule. Jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linalotua magharibi, Mwana wa Mungu aliwazukia watu wa mashariki. Alifanya nini kuwathibitishia Wasamaria na Wayahudi ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi? Kwa kuwaonyesha ishara, kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake.

<sup>108</sup> Yule mwanamke Msamaria alishuhudia jambo lile lile, akisema, “Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

<sup>109</sup> Akakimbia mjini na kusema, “Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi? Huyu Mtu aliniambia shida yangu, yale ninayofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Nao watu wakaamini hilo. Alifanya hivyo kwa Wasamaria na kwa Wayahudi, bali si kwa Mataifa, kabla Injili haijawaendea Mataifa Yeye alikuwa tayari ametukuzwa na yuko Utukufuni.

<sup>110</sup> “Lakini itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Kanisa lilifanya nini? Liliingia katika Ukatoliki, likauka kanisa; ndipo Luther akajiondoa kwa ajili ya kuhesabiwa haki, kwa ajili ya Uzao; kisha Wesley akatoka kwa Luther, utakaso; halafu Wapentekoste, nao wakaunda dhehebu, na kuendelea na kuendelea na kuendelea, mifumo yao, na kuendelea.

<sup>111</sup> Sasa tunafikia siku za mwisho, ni kitu gani? Lakini wakati wa jioni, kabla mwili wa Sara na Ibrahimu haujabadilishwa kumpokea mwana aliyeahidiwa, Yeye alikuja, akaketi pamoja nao, akazungumza nao, na kufanya ishara mbele yao; naye Yesu aliirejea. Hatuko nyuma, msiangalie nyuma yale Luther aliyosema, yale Wesley aliyosema, angalieni yale Yesu aliyosema, angalieni ishara mahali tulipo.



<sup>112</sup> Msiangalie nyuma, yale mtu mwingine aliyosema, angalieni yale Yeye aliyosema, Yeye Ndiye, aliyeyasema. Nalo jua lile lile linalochomoza mashariki, hutua magharibi. Kumekuwa na siku yenye utusitusi, bila shaka imekuwako, Nuru ya kutosha kuona jinsi ya kujiunga na makanisa na kuunda madhehebu na kadhalika.

<sup>113</sup> Lakini nguvu hizo halisi na madhihirisho ya Uwepo wa Mungu hazijaonekana kwa miaka na miaka na miaka. Tulizihisi, tunajua ya kwamba ziko hapa, tumeona karama zikifanya kazi nazo, bali tunapomwona Yeye akionekana wazi miongoni mwetu, pamoja na nguvu Kanisani Mwake kuunyoshea mkono upindo wa vazi la Bwana huyo na kuligusa, kuzishusha nguvu Zake hapa tena, na kunena kupitia watu Wake hapa na kufunua, ikimfanya Yeye Mungu, Mungu pamoja nasi! Loo, naam!

<sup>114</sup> Ewe Yohana, Mungu na afungue milango ya gereza usiku wa leo na akufungulie utoke. “Heri awaye yote, asiyechukizwa Nami,” si kusoma mawazo, au telepathia, bali nguvu za Kristo aliyefufuka, Ambaye yuaja hivi karibuni.

Na tuombe.

<sup>115</sup> Mungu mpendwa, wakati Nuru za jioni zinapoangaza, zinayapofusha macho ya wengi, bali wengine wanazitumia kuingia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba utazitoa Nuru za jioni tena, na kwa nanii, watu hawa wa jioni, na jalia waone nguvu za kufufuka Kwako, kwa kuwa Wewe ulisema, Mwenyewe, ya kwamba, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Nasi tunashangaa ni kazi gani ulizofanya. Ndipo tunaona katika Yohana mlango wa 5, kifungu cha 19, ya kwamba Wewe ulisema, “Sifanyi neno mpaka nimwone Baba akilitenda kwanza.” Ndipo Wewe uliahidi hilo, tunajua ni kweli.

<sup>116</sup> Sasa, kwa mara nyingine tena, Bwana, kisha imekamilika. Na jalia wengi wa akina Yohana ambao wamefungwa gerezani leo, wanaume na wanawake wazuri, wanaokujua Wewe kama Mwokozi wao, nao wamekuwa wakishangaa, Ee Mungu, jalia waone kwamba Wewe uko kwenye wakati uliopangwa hasa, uko kwenye wakati unaofaa. Tujalie, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>117</sup> Sasa, kabla tu hatujafanya wito wetu wa madhabahuni, nimechelewa kidogo tu usiku wa leo, nami nilifikiri jana usiku nilihubiri. . . Nitamwambia Billy hakika nimefaulu usiku wa leo. Aliniambia nisingeweza kuhubiri chini ya saa moja na nusu, lakini hakika niliumalizia wakati huo, kwa msaada wa Bwana.

<sup>118</sup> Sasa, ninaamini tuligawa kadi za maombi jana, ama, je, aligawa zozote leo? Ama, hizo zilikuwa ni zipi? Moja hadi mia moja, ninaamini alizigawa jana, sivyo? Hizo zilikuwa ni zipi? Za A? Za A. Vema. Tulianza wapi? Tulienda, tulianza moja jana, sivyo? Moja? Vema, hebu tuanzia nyuma yake. Hebu tuchukue,

hebu tuanzie, tulete yapata, wachache tu hapa juu, maana muda wetu una-...Hebu tuanzie themanini na-...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

119 Ni wangapi hawajawahi kuwa katika mmoja wa hii mikutano hapo kabla? Inueni mikono yenu. Angalieni tu kule, nusu ya mkutano. Ikiwa Yesu Kristo...Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu Kristo tayari amewaponya wagonjwa, tayari amewaokoa waliopotea? Sasa, Yeye asingeweza kukuokoa wala kukuponya, Yeye angekwambia tu tayari amefanya jambo hilo, huna budi kuamini.

120 Lakini Yeye aliahidi ya kwamba kazi alizofanya, tutazifanya pia, na hasa sana katika wakati huu wa jioni. Ni wangapi wanaojua hilo, wanaoamini hiyo ni kweli? Je, linasema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele?” Hakika ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Vema. Kama ndivyo alivyo, basi na atende hivyo.

121 Sasa, ninyi nyote mlio kwenye mstari wa maombi, mnaosimama hapo, ambao hatufahamiani, ambao mnajua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, wote wanaojua. Kila mmoja wao.

122 Vema, nyote huko nje, ninyi watu ambao hamna kadi ya maombi, nanyi mnataka kuponywa, nanyi mnajua sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, watu wote.

123 Kila mtu humu jengoni anayejua ya kwamba sijui lolote kukuhusu, inueni mikono yenu, kila mahali. Sidhani kuna mtu ambaye ninaweza kumwona ambaye namjua. Kama sijakosea, huyu ni mhubiri kutoka Arkansas, aliyeketi papa hapa, ninaamini. Nuru hizi, mnaona, si—siwezi kumwona vizuri sana, bali nafikiri huyo ni mhubiri kutoka Arkansas.

124 Ni wangapi wanaojua ya kwamba wakati mmoja kulikuwa na mwanamke aliyekuja kwenye mstari wa maombi? Kulikuwa na mama aliyeingia, akasema moyoni mwake, “Kama nikiweza tu kugusa upindo wa vazi la Mtu huyo, nitakuwa mzima,” alikuwa anatokwa na damu. Mnakumbuka hilo? Naye akajipenyeza kwenye umati, na kugusa, karibu *hivyo*. Sasa, kamwe usingehisi hilo. Nawe unajua, Ndugu Tommy, vazi la ndani la Mpalestina, lile joho kubwa refu, walivaa vazi la ndani kwenye namna fulani ya mavumbi, barabara ikiyaokota.

125 Sasa, kama aligusa upindo wa vazi hilo, akarudi kwenye kusanyiko...Naye Yesu akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Sasa, huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. “Ni nani aliyenigusa?”

126 Ndipo Petro akamkemea, kasema, “Vema, wote... itakuwaje...mbona, watu wanafikiri una kasoro fulani. Wao, mbona, wao, kila mtu anakugusa Wewe.” Mnajua, “Halo hapo. U hali gani, Kasisi?” na kadhalika, mwajua, “Rabi.”

127 Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu.” Ni wangapi wanaojua ya kwamba nguvu ni uweza? Bila

shaka. “Nguvu zilinitoka. Mtu fulani alinigusa Mimi.” Naye akageuka, akaendelea kuangalia juu ya hilo kusanyiko, mpaka akapata mahali ilipokuwa, Naye akasema, akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma kwa sababu imani yake ilikuwa imemwoko. Je, hiyo ni kweli?

Vema sasa, hivi Yeye, usiku wa leo, ninyi ndugu wahudumu, ambao tunakula nao asubuhi ya leo . . . ?

<sup>128</sup> Ndugu huyu *hapa*, ninaamini, ndiye ndugu ambaye alizungumza juu ya digrii zote alizo nazo, katika—katika—katika shule ya Kibaptisti, Daktari, na Ph.D., nami sijui yote hayo, aliyokuwa akitwambia habari zake, bali ilimbidi kusahau yote, kama Paulo, apate kumjua Kristo.

<sup>129</sup> Kwa hiyo, basi, lakini Maandiko yanatufundisha katika Waebrania ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa hivyo? Vema, basi kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angetendaje kama ungemgusa? Mnaona? Angetenda vivyo hivyo, sivyo? “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona; kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu; hata ukamilifu wa dahari; kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Hiyo ni kweli? Naye aliahidi hili lingewajia watu wa Mataifa, si kote katika Wakati wa Kilutheri, Wakati wa Wesley, bali katika wakati wa mwisho lingetukia.

<sup>130</sup> Sasa, hivi hamwoni? Yeye yuko kwenye wakati hasa, moja kwa moja, na kumbukeni, hili tayari limeenda kote ulimwenguni. Kwa hiyo tuko mwisho, hapana shaka, hapana shaka. Bali wewe gusa vazi Lake.

Sasa, “Ni kitu gani, Ndugu Branham?”

<sup>131</sup> Si mimi. Wala haingenifaa kitu kama hukufanya hivyo. Ni—ni wewe, unahusika tu kadiri ninavyohusika. Haina budi kuwa imani yako ndiyo inayofanya ninii Lake. . . inayomgusa, kusudi apate kunena kupitia kwangu. Ni karama tu kujitolea Kwake, kumpa tu macho yangu, akili zangu, ulimi wangu, utu wangu, sasa, simjui hata mmoja wenu, bali ni—ni Yeye akinena kupitia pale, mnaona. Ni Yeye anayefanya hivyo. Kwa hiyo si—si mimi. Kwa hiyo ni kitu gani kilicholisababisha kufanya hilo? Sikujui.

Unasema, “Kunihusu mimi, Ndugu Branham?”

Sijui.

“Kunihusu mimi?”

<sup>132</sup> Sijui, bali Yeye anajua, kwa hiyo unamgusa Yeye, ndipo Yeye ananitumia tu, tena. Kwa hiyo, unaona, ni mimi na wewe pamoja, kama watumishi Wake. Naye hujifanya Mwenyewe ajulikane kwa watu Wake, ya kwamba hajachelewa, Yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa, hasa, kabla tu ya wakati wa mwisho, wakati Nuru za jioni zingegangaza.

Sasa, kama atafanya hivyo, ni wangapi watakaompenda na kumwamini na kumkubali? Mungu awabariki.

<sup>133</sup> Sasa, Baba wa Mbinguni, yaliyosalia yako mikononi Mwako. Ninajikabidhi mwenyewe na kusanyiko hili Kwako. Kisa kimoja tu kitathibitisha hilo, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo, na litendeke. Amina.

<sup>134</sup> Sasa, iweni na kicho kabisa, msiinuke tena, tulieni kimya. Iweni na kicho kabisa kwa dakika chache tu.

<sup>135</sup> Sasa, Neno moja kutoka Kwake litamaanisha zaidi ya vile ningeweza kusema katika nyakati hamsini, mia moja za maisha, Neno moja tu kutoka Kwake.

<sup>136</sup> Sasa, ninyi huko nje sasa msio na kadi ya maombi, ama popote mlipo, hata hali yako iweje, wewe sema tu, “Ee Kuhani Mkuu, jalia nikuguse Wewe. Naye Ndugu Branham hanijui, na basi Wewe umgeuze kwangu, na jalia aniambie kile ninachoombea, jalia aniambie nina shida gani, yeye hanijui, hapa, loo, jambo ninalowazia, ama kufanya, ama chochote kile, hebu aniambie, nitakuamini Wewe.” Maana Biblia ilisema hivyo ndivyo tu Yeye angefanya. Hivyo ndivyo *alivyofanya*, hivyo ndivyo *atakavyofanya*.

<sup>137</sup> Nanyi mnaona, marafiki, kama mara moja ilimfanya Yesu ajisikie mnyonge, ingenifanyia nini mimi, mwenye dhambi? Kamwe hamtajua mpaka tutakapokutana langoni kule juu, yale mimi. . . ni nini. . . gharama yake. Lakini hilo, silalamiki, ninamshukuru Mungu, mnaona; kusudi tu mpate kufahamu.

<sup>138</sup> Vema, siku nyingi, tunakuja, nao wanasambaza kadi za maombi, na halafu baadaye, ninachukua kadi hizo za maombi kote, kote katika juma la—la kuchukua baadhi yake *hapa*, na zingine *huku*, na huku *chini*, kusudi isije, kila mtu asije akang’ang’ania kadi ya maombi namba moja. Mnaona? Kwa hiyo wao, na halafu, huyo mvulana, kabla hajazigawa, anashuka, na kusimama mbele ya kusanyiko, na kuzichanganya kadi hizi, anazichanganya zote. Nadhani mmemwona akifanya hivyo. Vema.

<sup>139</sup> Kisha anashuka, ukitaka moja, anakupa moja. Ndipo huyo mvulana hawezi kusema, “Vema sasa, nilimpa namba moja.” Yeye mwenyewe hajui, anazigawa tu, mnaona, anazichanganya, anakupa, huenda akakupa kumi, naye huyo mwingine karibu nawe, tisini na tano.

<sup>140</sup> Kwa hiyo basi, mahali fulani kote katika juma hili, ninaweka, nitaita kuanzia ishirini hadi thelathini, ama kutoka hamsini hadi tisini, ama tisini kurudi nyuma hadi ishirini, ama mahali fulani namna hiyo, popote Bwana anapoweka moyoni mwangu, maana, kwa njia hiyo, mbona basi, popote tu Roho Mtakatifu anapoongoza kuitia.

141 Imetokea kuwa usiku wa leo, kwa uongozi huo, mwanamke huyu, mwanamke mweusi, mimi, mzungu. Hivi mimi ni mgeni kwako? Hatufahamiani? Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana?

Mnaona sasa?

142 Sasa, kama Roho Mtakatifu, angali anabaki Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani ya Kristo, akiwa ndani yetu usiku wa leo, kama huyo ni Roho yeye yule, basi atafanya kazi ile ile. Kama hili ni kweli, Roho Mtakatifu, basi atafanya kazi ya Roho Mtakatifu, kama . . . Atafanya kazi ya Yesu.

143 Na kwa njia hiyo unaweza kuwa na hakika, basi, kile alichokuwa huko nyuma, unajua kile alichosasa. Kwa hiyo hebu tuchukue Yohana Mtakatifu mlango wa 4, kulikuwako, wakati Yeye, akiwa ni Myahudi, alipokutana na mwanamke Msamaria, naye akazungumza naye dakika chache apate kuishika roho yake, ndipo akamwambia mahali shida yake ilipokuwa. Naye akasema, “Bwana, naona ya kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya.” Naye akamwambia *hivyo*.

Naye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

144 Ndipo akakimbia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Nao watu wote wakaamini, na kila mmoja, Yesu hakufanya hivyo kwa mtu mmoja zaidi, lakini mji mzima ukamwamini Yeye. Hakumponya mtu yeyote, aliingia tu mle, akajitangaza Mwenyewe. Yule mwanamke . . . Nayo Biblia ilisema ya kwamba mji mzima ulimwamini kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke.

145 Sasa, kama huyo alikuwa ni Yesu jana, Naye anaweza kuja kufanya jambo lile lile, kama vile msichana Mwafrika na mwanamume Mwanglo-Sakson waliosimama hapa, na kama anaweza kunifunulia jambo ambalo limekuleta hapa, jambo ambalo umefanya, ama kitu kama hicho, unajua—unajua kama ni kweli ama si kweli. Bila shaka ungefanya hivyo. Halafu basi, kama anaweza kukwambia yale yamekuwako, bila shaka Yeye anaweza kukwambia yatakatotukia. Unaamini hilo?

146 Kwa watu wote weusi hapa, wazungu pia, na wowote wale, mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? Vema.

147 Sasa, kama yeyote wenu ninyi watu hamwamini hili ni kweli, na mnaamini ni saikolojia, sina Ph.D., wewe njoo hapa na ufanye hivyo mwenyewe.

148 Ninakungojea.

149 Basi kama unaogopa kuja, likubali, ama ulinyamazie, unaona.

150 Nilisema hivyo kwa sababu niliongozwa kufanya hivyo. Kuna jambo fulani linaloendelea ambalo ni—ninajua habari zake.

151 Wewe unajua ya kwamba jambo fulani linaendelea *hapa*, pia. Moja ya shida zako ni wasiwasi, wasiwasi kupindukia.

152 Hiyo hapo inakuja, “Alibahatisha hilo.” (Hivi, mnalipata hilo sawa?) Ningeweza kusema, “Mtu fulani huko nje ana wasiwasi, mtu fulani, Bwana alisema jambo fulani,” lakini huyo mtu ni *nani*? *Huyu* ndiye yule mtu fulani.

153 Simama. . . Yeye ana roho nzuri, tunaona ya kwamba huyu ndiye. Wasiwasi? Una shida na bega lako pia. Hiyo ni kweli. Una ugonjwa wa moyo pia. Hiyo ni kweli? Una mzungu moyoni mwako. Hiyo ni kweli? Ni kuhusu mvulana fulani. Uh-huh. Yuko kwenye, taasisi ya vichaa, hospitali, unamwomba. Unanitaka, nikwambie wewe ni nani? Bibi Richardson, nenda, amini.

154 Kamwe hamtajua hilo linanifanyaje, linaua tu uhai wenyewe. Sasa, kwa uchaji kabisa, kila mmoja.

155 U hali gani, bwana? Hatufahamiani, hatufahamiani, bali Yesu anatujua sote wawili na ametulisha sote wawili. Kama Mungu atanijalia tu kujua sababu ya wewe kusimama hapa, kusudi isinibidi kueleza kwa utondoti mwingi mno. Unaona, wote, tuna mstari mzima wamesimama hapo, na wengine huko nje wakiomba. Mnaona jinsi inavyonifanyia.

156 Lakini kama Yeye angeniambia tu jambo fulani kukuhusu, ungeamini? Bila shaka, moja ya mambo unayotaka kuomba ni macho yako, bila shaka, umevaa miwani, mtu yeyote anaweza kuona hilo.

Hiyo siyo shida tu ya huyu mwanamume. Kuna kitu kingine, kwa sababu ana uvuli juu yake wa mauti, macho yake yasingefanya hivyo.

157 Ni TB, kifua kikuu, ulifanyiwa upasuaji kwa ajili yake, haukufanikiwa, haujafanya jinsi ulivyopaswa kufanya. Hiyo ni kweli? Unaamini sasa, itakuwa sawa? Amini tu kwa moyo wako wote.

158 Je, ungeamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu na alikuponya? Je, . . . Ungeamini? Basi pitia tu hapa, ukisema, “Asante, Bwana.” Kidonda hicho kitapona.

159 Sikujui. Hatufahamiani. Unamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu? Unaamini Yeye alinituma kama mjumbe kwa Kanisa katika siku hizi za mwisho, kuyaleta Maandiko haya na kutoa karama? Si kwa sababu ilikuwa ni mimi. Si kwa sababu ilimbidi kupata, Yeye alikuwa. . . Yeye labda, kwa kawaida humpata mtu fulani, asiyejua chochote, kusudi aweze kujionyesha Mwenyewe. Unaona? Unaamini ya kwamba mambo haya ninayonena ni kweli kwa Maandiko?

Anaonekana kuwa amejaa huzuni sana ndiyo sababu ni—nilikuwa nikiongea naye kwa dakika moja.

<sup>160</sup> Naam, ndivyo ilivyo, jambo la kwanza ni kwa ajili yako mwenyewe, umefanyiwa u—upasuaji. Na hiyo ilikuwa ni ya kike, shida ya kike, kuondolewa uchafu kwa kusafishwa kwa sehemu ya ndani ya viungo vyote vya kike. Lakini u—ukaenda vinginevyo, ukafanya jambo fulani. Sasa, hebu kidogo. Ni . . . dak- . . . imepasuka, ilipasuka na ikakubidi kurudi, ilibidi urudi tena.

<sup>161</sup> Lakini ninii yako—yako, hiyo kweli siyo huzuni yako. Huzuni yako ni kuhusu mtoto, ni mtoto wako. Na—naye amekuwa na ugonjwa fulani, ama kasoro fulani, TB. Na sasa ana namna fulani ya vipindi vya udhaifu, hiyo ni kweli. Una mwingine unayesumbuka kumhusu, naye ana ugonjwa wa sikio. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bibi Smith. Nenda zako, mwamini Bwana na itakuwa . . . ? . . .

Unaamini? Amini. Ku—kuwa tu na imani, amini.

<sup>162</sup> U hali gani, mama? Hatufahamiani. Si—sikujui. Nijuavyo mimi, sijawahi kukuona maishani mwangu, nasi tumekutana tu hapa kwa mara ya kwanza. Kama ni—kama ningeweza kukufanyia jambo fulani na nisingelifanya, basi ningekuwa—ningekuwa mtu mbaya, Mimi si—si, sipaswi kuwa nimesimama nyuma ya mimbara hapa kama mhudumu.

<sup>163</sup> Na mimi—mimi nisingeweza kukusaidia. Na kama alikuwa amesimama hapa Mwenyewe, na amevaa nguo hizi alizonipa, angeweza tu kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Masihi ambaye alikuwa amekufanyia, bali ingekubidi kuaimini ya kwamba Yeye alikufanyia hilo, la sivyo li—lisingefanya kazi kwa vyovyote vile. Hiyo si ni kweli? Lakini kama Yeye angesimama hapa na kukwambia jambo fulani, kwamba shida yako ni nini, ama yale uliyofanya, yale hukupaswa kufanya, ama jambo fulani kulihusu, basi ungekuwa na imani ya kuamini, sivyo?

Hilo lingeinua imani ya hili kusanyiko sasa? Wewe unafifia kwangu.

<sup>164</sup> Vema, ulipata ajali, ukasumbuka kichwani. Halafu basi una shida katika upande wako wa kushoto. Hiyo ni kweli. Matatizo, mambo mengi sana mabaya. Hiyo ni kweli. Naam, mama. Kama Mungu angeniambia wewe ni nani, ingekusaidia? Bibi Terry. Mungu akubariki.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa?

Yeye huonya ugonjwa wa moyo, sivyo? Unaamini Yeye huonya? Endelea tu moja kwa moja ukisema, “Asante, Mungu mpendwa, asante.” Naam, bwana.

Unaamini Yeye huonya yabisi kavu na kuwapa watu afya? Vema, njoo tu, amini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki.

Ugonjwa wa akina mama na ugonjwa wa moyo. Unaamini Yeye atakuponya? Vema. Nenda zako moja kwa moja ukishangilia, ukisema, “Asante.”

Wewe ni mdogo kuwa na ugonjwa wa upungufu wa damu, lakini je, unaamini Yeye hutia damu? Nenda, useme, “Asante, Bwana.” Nenda, ukiamini.

Uvimbe puani na kila ninii, loo, unaamini Yeye huuponya? Nenda tu, useme, “Asante, Bwana Yesu.”

<sup>165</sup> Itakubidi kufanyiwa upasuaji wa uvimbe huo, lakini unaamini Mungu atakuponya huo? Vema, vema, nenda zako tu moja kwa moja ukishangilia, ukisema—ukisema, “Asante, Bwana.”

Njoo. Njoo, mama. Unaamini Yeye huuponya wasiwasi? Vema, nenda zako ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.” Amina.

Vipi kama sikukwambia chochote? Je, ungeniamini hata hivyo? Njoo hapa. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Nenda, ukiamini.

Njoo. Hebu kidogo, kidogo tu, jambo fulani lilitukia mahali fulani.

Je, hao watu waliokuwa wakipitia pale, waliokuwa kwenye mstari wa maombi, walirudi kule nyuma? Loo, naam. Huenda hilo lilikuwa ndilo . . .

<sup>166</sup> Bwana, uliyeketi papa hapa kwenye safu, uliyeketi papa hapa ukiniangalia, unaugua ugonjwa wa tezi dume. Naam, bwana. Uliyeketi hapo, naam, bwana. Um-hum. Naam. Je, una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi, sivyo? Huihitaji, imani yako ilikuponya.

<sup>167</sup> Mwanamke huyu wa pili kutoka hapo, ni mke wako. Hiyo ni kweli. Ninawaona katika nyumba fulani pamoja. Naye anaugua ugonjwa wa ini lake. Hiyo ni kweli. Kama ni kweli, inua mkono wako. Nendeni nyumbani, Yesu Kristo amewaponya.

<sup>168</sup> Huyo mama aliyeketi hapo, karibu nawe, ana kasoro kwenye ulimi wake. Unaamini, mama? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Nenda nyumbani.

<sup>169</sup> Wewe, uliyeketi mwishoni huko nje, nawe je? Hiyo hapo juu yako sasa, una ugonjwa wa kibofu. Hiyo ni kweli. Vema. Unaamini? Vema, nenda nyumbani ukawe mzima.

Unaukubali? Waligusa nini?

<sup>170</sup> Hapa—hapa ameketi mtu aliyeanza kulia, aliyeketi papa hapa nyuma, mtu huyu, ni yule jamaa mdogo. Sasa, mtu huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini sikiliza, mwanangu, una ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Lakini ulikuwa unaomba, Roho akaja juu yako, hisia nzuri sana. Kama hatufahamiani, pungua mkono wako *hivi*. Sikujui. Je, hiyo ndiyo



shida yako? Punga mkono wako. Vema, umeponywa. Yesu Kristo anakuponya.

<sup>171</sup> Mama huyu aliyeketi moja kwa moja huko nyuma, akiagua kifafa, unaamini ya kwamba Mungu atakupa afya, akuponye? Unaamini hilo? Kama utakubali uponyaji wako, hivyo vipindi vitakuacha, hutakuwa navyo tena. Amini.

<sup>172</sup> Maskini huyo mama, aliyeketi hapo, akiniangalia kando huku ameinua mkono wake *hivi*, shida na kifundo chake cha mguu, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, unaweza kupokea uponyaji wako.


<sup>173</sup> Huyu mama aliyesimama hapa umeinua mkono wako, uko tayari kwa ajili ya upasuaji, maskini uvimbe huo, bali Mungu atauondoa, akupe afya. Unaamini? Nenda, amini hilo.

Mwanamke huyu mwema, mwenye ukanda mweupe kichwani mwake hapa, mama mweusi, ugonjwa wa kibofu nyongo. Unaamini Mungu atakuponya?

<sup>174</sup> Vipi kukuhusu wewe kwenye kiti cha magurudumu? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Utakufa ukiketi hapo. Una nafasi moja ya kuishi, kama wale wenye ukoma walivyokuwa, walioketi kwenye lango la Samaria. Siwezi kukuponya, Dada, mimi si mponyaji. Lakini wale Wasamaria, walisema, “Tukiketi hapa, tutakufa, tukienda mjini, tutakufa. Kwa hiyo nafasi pekee tuliyo nayo ni kwenda kwenye kambi ya adui, kama wakituua, tutakufa kwa vyovyote vile, lakini wakituokoa, tutakuwa hai.”

<sup>175</sup> Walikuwa na nafasi moja kati ya mamilioni. Huna nafasi ya namna hiyo, umealikwa, usiku wa leo, kwenye Nyumba ya Mungu mwenye upendo halisi. Simama kwa miguu yako sasa. Nenda, tembea hata hivyo.

<sup>176</sup> Hebu tuinuke na kumwamini Bwana Yesu Kristo. Simameni. Kama utamwamini, simama kwa miguu yako, katika Jina la Yesu Kristo, na ukubali uponyaji wako. Amina.

(Chukua wito wa madhabahuni.) 

61-0425E Heri Iliyosahaulika  
Stephen Mather High School  
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)